

**AMRI YA DHARURA #**  
**Kurudi kwa Melesi**

**AMBAPO**, mnamo Desemba, 2019 aina mpya ya virusi vya corona viligunduliwa, sasa vinaitwa COVID-19, na vimeenea ulimwengu kote, ikiwa ni pamoja na kila jimbo Marekani.

**AMBAPO**, mnamo Januari 30, 2020, Shirika la Afya ya Ulimwengu ilitangaza COVID-19 kuwa Jambo la Dharura la Afya ya Umma la Kuhusika Kimataifa.

**AMBAPO**, mnamo Machi 12, 2020, Gavana Tony Evers alitangaza dharura ya afya ya unna na kuagiza shirika zote kusaidia juhudzi za kuitikia na kuthibiti COVID-19 katika Winsconsin;

**AMBAPO**, mnamo Machi 13, 2020, Rais Donal Trump alitangaza Dharura ya Taifa kuhusu COVID-19;

**AMBAPO**, kufikia Aprili 19, 2020, watu 2,241,359 kote ulimwenguni wamepimwa kuwa na COVID-19, ikiwa ni pamoja na 690,714 katika marekani na 4,346 katika Winsconsin;

**AMBAPO**, COVID-19 inapatikana kote Winsconsin, huku watu wakipatikana kuwa na COVID-19 ndani ya kaunti 65 za 72 kufikia Aprili 19, 2020;

**AMBAPO**, mnamo Machi 24, 2020, mimi, Andrea Palm, Katibu Mkuu wa Idara ya Huduma za Afya ya Winsconsin nilitoa Amri ya Dharura #12, Amri ya Salama Nyumbani(sasa na baadae “Amri ya Salama Nyumbani”), inayohitaji kuwa kila mtu katika Winsconsin akae nyumbani mwao au pahali pa makazi isipokuwa katika hali chache;

**AMBAPO**, mnamo Aprili 16, 2020, nilibadilisha na kuongezea Amri ya Salama Nyumbani ili kuwezesha mabiashara kupata fursa mpya kurudi kazini na kuweka hatua mpya za kuweka wafanyakazi na wateja salama;

**AMBAPO**, Amri ya Salama Nyumbani inafanya kazi ili kunyoosha mkunjo wa maambukizi ya COVID-19 katika Winsconsin, na tumeanza kuona matokeo ya maana kutokana na hatua hii nzuri;

**AMBAPO**, tunajua ya kwamba Amri ya Salama Nyumbani inafanya kazi ili kuzuia maongezeko katika kesi za COVID-19 ambazo zinaweza kuzorotesha mfumo wetu wa afya na kuhatarisha maisha zaidi;

**AMBAPO**, pamoja na maendeleo ambayo Wisconsin imeifanya katika kunyoosha mkunjo na kupunguza kuenea kw COVID-19, ni lazima tutazame mbele na kuganga jisi Winsconsin itarudia biashara kama kawaida;

**AMBAPO**, Miongozo ya Rais Donald Trump ya Kufungua Marekani Tena, iliyotolewa Aprili 16, 2020, inatoa mfumo kamili na wenyewe maana wa kuanza upya uchumi bila kutoa sadaka ya mapato ya afya ya umma ambayo tumepata katika kupambana na ugonjwa huu;

**AMBAPO**, kungozwa na sayansi, ukweli wa afya ya umma ulio sakafuni, na mwongozo kutoka serikali ya Shirikisho, Amri hii inatekeleza njia ya kufanya na kuzuizi cha Amri ya Salama Nyumbani; na

**AMBAPO**, tumeona hali ya afya ya umma inweza kubadilika haraka nahii jia itawaruhusu watu na mabiashara nafuu zaidi wakati wa kuhasibu hali ya kutokuwa na hakika kutokana na janga hili.

**SASA BASI, Mimi, Andrea Palm**, Katibu Mkuu, Idata ya Huduma za Afya, kwa mamlaka iliyowekwa ndani yangu na sheria za Jimbo ikiwa ni pamoja na, wala sio tu Sehemu 252.02(3), (4), na (6)ya Sheria za Winsconsin, naamrisha yafuatayo:

- 1. Awamu.** Winsconsin itachukua hatua ya awamu ya kufungua tena uchumi wake na jamii, na kila awamu ikiwa ikizidi kuzuia biashara na watu na wakati huo kukinga umma kutokana na COVID-19. Idara ya Huduma za Afya inatangaza mabadiliko kwa kila Awamu na amri inayoeleza kabisa shughuli zitakazo rudishwa. Awamu zinajumuisha:
  - a. Salama Nyumbani.** Inaendelea sasa kama iliyovoanzishwa katika Amri za Dharura #12 na #28.
  - b. Awamu ta Kwanza.** Awamu ya kwanza itajumuisha kukubalisha makongamano ya idadi ya watu hadi 10; mahoteli yatafunguliwa na mahitaji ya kujitenga kijamii, kutolewa kwa vizuizi Fulani ikiwa ni pamoja na vizuizi vya kuuza kwa Biashara na Shughuli Muhimu; shughuli za ziada za bishara zisizo muhimu; Shule za K-12 kufunguliwa kwa shughuli za watu kukaa ndani na mipango ya kutunza mtoto yarejee kikamilifu.
  - c. Awamu ya Pili.** Awamu ya pili itajumuisha kukubalia mikongamano ya idadi wa watu hadi 50; mahoteli kufunguliwa kabisa; baa kufunguliwa na kahitaji ya kujitenga kijamii; bishara zisizo muhimu kurejesha shughuli na mahitaji ya kujitenga kijamii; na masomo ya baada ya shule ya upili yanaweza kurejesha shughuli.

**d. Awamu ya Tatu.** Awamu ya tatu itarejesha shughuli zote za biashara na makongamano, ikiwa ni pamoja na hatua kiasi za kukinga na kuzuia zikipatikana kwa umma na hatua zaidia za kukinga kwa idadi ya watu katika mazingira magumu.

**2. Maendeleo kupitia Awamu hizi.** Idara ya Huduma za Afya itatathmini habari mpya ya kisasa ili kuona ni lini inafaa kuendelea na Awamu inayofuata. Kuendelea kwa Awamu inayofuata, serikali lazima ifanye maendeleo kuelekea malengo yaliyotambuliwa hapa chini kama Majukumu ya Msingi na Kigezo cha Kuingia.

**a. Majukumu ya Msingi.** Serikali lazima ionyeshe maendeleo katika sehemu zifuatazo:

**i. Upimaji.** Kila mkazi wa Winsconsin aliya na maradhi ya COVID-19 ana ufikiaji wa mapimo ya maabara. Matokeo yataripotiwa kwa mgonjwa na maafisa wa afya ya umma katika masaa 48 ya kuchukuliwa. Malengo ni kufanya takriban mapimo 85,000 kila wiki au 12,000 kila siku.

**ii. Kufuatilia.** Zidisha kufuatilia kwa mawasiliano ya idadi ya watu hadi 1000 na kutekeleza suluhu za kiteknologia ili kuhakikisha kila ambaye ameambukizwa atajitenga au kwenda karantini kwa usalama.

**iii. Ufuatiliaji.** Kujenga juu ya mifumo inayotumia kufuatilia ugonjwa wa mafua na janga la COVID-19 na kuripoti kwa Kigezo cha Kuingia cha Winsconsin na metri zingine husika.

**iv. Vifaa vya Kibinasfi vya Kujikinga (PPE).** Nunua PPE na bidhaa zingine zinazohitajika kusaidia utunzaji wa afya na mashirika ya usalama wa umma.

**v. Uwezo wa Utunzaji wa Afya.** Tathmini hitaji na utayari wa kusaidia uwezo wa ongezeko kwa mfumo wetu wa huduma ya afya.

**b. Namna ya Kuzuia.** Serikali lazima ifuate Namna ifuatayo ya Kuzuia, kulingana na harari za afya ya umma za kote nchini.

**i. Maradhi:**

**1.** Utaratibu wa kushuka wa magonjwa kama ya mafua yaliyoripotiwa katika kipindi cha siku 14; na

**2.** Utaratibu wa kushuka wa magonjwa kama ya COVID-19 yaliyori potiwa katika kipindi cha siku 14;

**ii. Kesi:** Utaratibu wa kushuka wa kesi hakika kama asilimia ya kesi jumla zilizopimwa katika kipindi cha siku 14: na

**iii. Hospitali:**

- 1.** Matibabu ya wagonjwa wote bila utunzaji wa shida;
- 2.** Mipango mikubwa ya kupima inapatikana kwa wafanyakazi wa ujinzaji wa afya walio kwenye hatari: na
- 3.** Kupunguza idadi ya wafanyakazi wa utunjazi wa afya walioambukizwa.

**3. Maendeleo ya muda katika Awamu.** Kwa kuongeza kwa kuendelea katika kila awamu hapo juu, Idara ya Huduma za Afya, kwa kushaurina na Shirika la Maendeleo ya Uchumi la Winsconsin, itatoa amri zaidi za kupunguza vizuizi katika mabiashara au sekta Fulani ikiwa itadhibitishwa kwamba kutoa vizuizi hivyo kutakuwa na athari kidogo kwa uwezo wan chi wa kutekeleza Majukumu ya Msingi na Kigezo cha Kuzuia.

**4. Amri za mtaa.** Idara ya Huduma za Afya, kwa kushauriana na maafisa wa afya wa eneo hilo, wanaweza kushughulikia milipuko ya kawaida na amri ya mahali hapo. Amri kama hiyo inaweza kujumuisha kurekebisha Awamu au kuanzisha vizuizi vilivyowekwa kulingana na mahitaji ya eneo fulani, kaunti, au eneo.

**5. Salama Nyumbani inaendelea kutumika.** Hakuna chochote katika Amri hii kinachorekebisha, kubadilisha, au kuzidi Amri ya Dharura #28, Walakini, Amri ya Salama Nyumbani inaagiza kuanzisha awamu hizo chini ya kifungu cha 2 na maagizo ya muda ya kupunguza vikwazo chini ya kifungu cha 3 yanaweza kutolewa kabla ya kumalizika kwa Amri ya dharura #28, ikiwa inafaa chini ya vigezo vilivyotajwa hapo juu.

**6. Ukali.** Ikiwa utoaji wowote wa Amri hii au matumizi yake kwa mtu ye yeyote au hali yoyote itafanywa kuwa sio sawa, basi mabaki ya Amri, pamoja na utumizi wa sehemu hiyo au utoaji kwa watu wengine au hali, haitaathiriwa na litaendelea kamili nguvu na athari. Kwa maana hii, vifungu vyaa Amri hii vinaweza kuadhibiwa.

**7. Ukuu.** Amri hii linapitisha agizo lolote la mtaa ambalo linapingana na Amri hii.

---

Andrea Palm  
Katibu mteule  
Idara ya Huduma za Afya  
Jimbo la Wisconsin

---

Tarehe